East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 5, Issue 1, 2022
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Ubadili Maana katika Leksia za Kĩĩtharaka: Mtazamo wa Kifonolojia na Kimofolojia

*Kimathi Mwembu[1*], Allan Mugambi[2] & Timothy Kinoti M'Ngaruthi[3]*

[1] Chuo Kikuu cha Tharaka, S. L.P. 193– 60215, Marimanti, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Chuka, S.L.P. 109– 60400, Chuka, Kenya.
[3] Chuo Kikuu cha Embu, S.L.P. 6– 60100, Embu, Kenya
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0001-9687-2484; Barua pepe ya mawasiliano: kwamwembu@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.860**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*26 Septemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Kĩĩtharaka, Leksia, Ubadili Maana, Leksika-Pragmantiki.*

**IKISIRI**

Makala haya yanalenga kubainisha jinsi ubadili katika vitamkwa na mofu unavyoathiri maana ya leksia katika Kĩĩtharaka. Maana katika leksia hutegemea kipengele cha kiisimu na vile vile kile cha kijamii ili ieleweke vilivyo. Katika hali hii, mabadiliko ya kifonolojia, kimofolojia, pamoja na kileksia yanayoathiri maana yameangaziwa. Data ya kimsingi kutoka wazungumzaji asilia wa Kĩĩtharaka, imechanganuliwa kwa kutumia nadharia ya Leksika-Pragmantiki. Makala haya yanabainisha ubadili wa kifonolojia pamoja na kimofolojia ambao huchangia katika kuibuka kwa maana fulani katika leksia za Kĩĩtharaka. Makala haya yanabainisha kwamba maana katika leksia za Kĩĩtharaka hutegemea kwa njia moja au nyingine mabadiliko yanayohusisha usilimisho, kuimarika na kudhoofika kwa fonimu, uchopekaji, uyeyushaji, hapololojia, kanuni ya Dahl na Ganda. Aidha, ubadili unaoathiri maumbo ya mofu huchangia pakubwa kutokea kwa maana katika leksia. Mofu za ngeli, ukanusho na uambishaji ni miongoni mwa zile ambazo zimebainika kuathiriwa na ubadili, ambao huzua maana fulani. Makala haya yanahitimisha kwamba, maana ya leksia huwa na misingi yake katika kiwango cha fonimu na mofimu zinazotumika kuunda neno. Pia, kuna mwingiliano baina ya maana kimatumizi na maana kimuktadha wa leksia.

**APA CITATION**

Mwembu, K., Mugambi, A. & M'Ngaruthi, T. K. (2022). Ubadili Maana katika Leksia za Kĩĩtharaka: Mtazamo wa Kifonolojia na Kimofolojia. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 353-362. https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.860.

**CHICAGO CITATION**

Mwembu, Kimathi, Allan Mugambi and Timothy Kinoti M'Ngaruthi. 2022. "Ubadili Maana katika Leksia za Kĩĩtharaka: Mtazamo wa Kifonolojia na Kimofolojia". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 353-362. https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.860.

**HARVARD CITATION**

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Mwembu, K., Mugambi, A. & M'Ngaruthi, T. K. (2022) "Ubadili Maana katika Leksia za Kîîtharaka: Mtazamo wa Kifonolojia na Kimofolojia", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 353-362. doi: 10.37284/eajss.5.1.860.

**IEEE CITATION**

K. Mwembu, A. Mugambi, & T. K. M'Ngaruthi, "Ubadili Maana katika Leksia za Kîîtharaka: Mtazamo wa Kifonolojia na Kimofolojia", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 353-362, Sep. 2022.

**MLA CITATION**

Mwembu, Kimathi, Allan Mugambi & Timothy Kinoti M'Ngaruthi. "Ubadili Maana katika Leksia za Kîîtharaka: Mtazamo wa Kifonolojia na Kimofolojia". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Sep. 2022, pp. 353-362, doi:10.37284/eajss.5.1.860.

## UTANGULIZI

Kwa mujibu wa uainishaji wa Guthrie (1970), Kîîtharaka kimo katika kundi la lugha za Kibantu zinazopatikana katika eneo la Kati ya Kenya. Katika mgawo huu, Kîîtharaka kimepewa kodi ya E50. Bennet (1977, 1985) anasema kwamba kundi hili la lugha za Kibantu za eneo la kati ya Kenya hujulikana kama Lugha za Thagicu. Bennet (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa lugha za jamii-lugha ndogo ya Thagicu ni Kîîtharaka, Kikuyu, Kikamba, Kiembu na Kimeru. Kîîtharaka kina lahaja nne za kijiografia: Gîgatue, Kîîgoki, Gîntugî na Kîthagicû (Bible Translation and Literacy, 2010).

Maana katika leksia za lugha hutegemea mambo kadha wa kadha. Muktadha wa kiisimu na kijamii ni mojawapo wa vipengele vinavyoathiri uelewa wa maana ya leksia za lugha. Kubadilika kwa kitamkwa katika neno fulani kunasababisha kubadilika kwa umbo la neno husika. Kubadilika kwa leksia kifonolojia na kimofolojia kunazua athari katika maana ya neno, iwe ni kwa njia ya moja kwa moja au isiwe ya moja kwa moja. Makala haya yanadhamiria kuweka wazi jinsi ubadili unaojitokeza katika vitamkwa, mofu, pamoja na leksia za Kîîtharaka unavyoathiri uelewa wa maana katika mawasiliano.

## UBADILI WA KIFONOLOJIA KATIKA KÎÎTHARAKA

Athari inayotokea katika lugha ikihusisha fonimu moja au zaidi huwa ni ubadili wa kifonolojia.

1 (a). Bantû aaga i **gwa** Kinyua
Mahali hapa ni pa Kinyua

(b). Bantû aaga i **kwa** Njeru
Mahali hapa ni pa Njeru

Ubadili wa kifonolojia unaweza kugusa vipandesauti kama vile: irabu, konsonanti, fungu la sauti katika neno, silabi pamoja na sifa nyingine za kiarudhi. Ubadili wa kifonolojia unaathiri usarufi wa leksia na utamkaji wake, na kwa njia hii, maana ya neno huathirika; hata ikiwa huenda athari ile isiwe ya moja kwa moja katika leksia husika. Hata hivyo, kuna wakati ambapo maneno hukumbwa na mifanyiko ya kifonolojia na kisha kukatokea ubadili wa kisemanti (Gichuru, 2020). Mifanyiko ya kifonolojia huzuka katika lugha ili kuleta iktisadi katika nguvu inayotumika kutamka sauti husika (Mgullu, 1999). Uelewa wa ubadili wa kifonolojia ni muhimu kwa kuwa utasaidia kujua misukumo inayosababisha baadhi ya leksia kukumbwa na ubadili maana. Sehemu inayofuata imeshughulikia ubadili wa kifonolojia unaobainika katika Kîîtharaka.

### Kuimarika kwa Fonimu

Mfanyiko wa kuimarika kwa fonimu huhusisha sauti kubadilika kutoka kwenye sauti ambayo hutumia nguvu kidogo zaidi na kuwa sauti ambayo inatumia nguvu nyingi zaidi (Mgullu, 1999; Crowley na Bowern, 2010). Katika hali hii, sauti huwa katika ngazi tofauti kwa kutegemea nguvu inayotumika kuzitamka. Sauti sighuna hutumia nguvu nyingi kutamkika ikilinganishwa na sauti ghuna. Hivi ni kusema kwamba, sauti sighuna ni imara ikilinganishwa na sauti ghuna. Ubadili wa kifonolojia wa aina hii hutokea katika Kîîtharaka kwa namna zifuatazo:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.860

Katika (1b) kuna ubadili wa fonimu kwa namna ambavyo fonimu /ɣ/ inaimarika inapobadilika na kuwa /k/. Katika mpangilio wa ngeli za nomino, neno *bantû* [banto] linapatikana katika ngeli 16 ambapo kiambishi kiwakilishi cha ngeli hii ni {ɤa}. Hii ndiyo sababu kuna neno ***aaga*** [a:ɤa] katika (1a & b) linaloashiria mahali dhahiri. Katika muundo ndani wa (1b) tunatarajia kupata: *Baantu aaga i gwa Njeru*. Hata hivyo, kunatokea mfanyiko katika kivumishi kimilikishi [*ɤwa*] ambapo sauti /ɣ/ inajitokeza kama /k/ katika muundo nje. Katika hali hii, muundo nje wa 1 (b) ni: *Baantu aaga i kwa Njeru*. Kimsingi muundo wa kivumishi kimilikishi katika 1(a) ndio unatarajiwa kutokea. Hata hivyo, kutokana na kuwepo kwa neno *Njeru*[nɟɛru] ambalo linaanza kwa kikocha cha sauti ghuna /nɟ/; kimilikishi *gwa* [ɤwa] kilichoundwa na sauti tangulizi /ɣ/ ambayo ni ghuna inalazimika kuwa sauti /k/ ambayo sighuna.

Ubadili wa sauti /ɣ/ hadi kuwa /k/ katika kimilikishi *gwa* [*ɤwa*] hautokeikatika nomino pekee bali pia katika upatanisho unaohusisha vitenzi. Sentensi (2) zinatoa mfano kutoka Kĩĩtharaka.

2 (a). Bakûthi **gwa** Cianthî
‘Wameenda kwa Cianthî’

(b). Tûkûrîma **gwa** Gîtonga
‘Tumelima kwa Gîtonga’

(c) Bariina **kwa** Mutegi
‘Wanaimba kwa Mûtegi’

(d) Akarea **kwa**Îraûka
Atakula kwa Îraûka’

Katika (2c&d) sauti /ɣ/ inaimarika inapobadilika ili iwe /k/ licha ya kwamba kimilikishi kinatumika kuashiria ni wapi kitendo kilitokea bila kuhusisha nomino katika ngeli 16 kama ilivyo katika (1a&b). Kimsingi, hali inapaswa kuwa hivi:

| **Umbo ndani** | | **Umbo nje** |
|---|---|---|
| **g**wa Cianthî | → | **g**wa Cianthî |
| ***g****wa*Mûtegi | → | ***k****wa* Mûtegi |
| ***g****wa*Îraûka | → | ***k****wa* Îraûka |

Katika mifano hii, sauti /ɣ/ katika kimilikishi #*gwa*# hubadilika kuwa sauti /k/ ikiwa nomino inayorejelea mmiliki inaanza kwa sauti ghuna, na inabaki vivyo hivyo ikiwa nomino inayotaja mmiliki inaanza kwa sauti si ghuna. Katika hali hii, maana ya “gwa” na “kwa” ni moja. Kwa hivyo, sauti /k/ na /g/ huwa katika mpishano huru.

**Kudhoofika kwa Fonimu**

Mfanyiko huu unasababisha fonimu inayotumia nguvu nyingi kuwa, yaani sauti hafifu kubadilika kuwa ghuna. Sauti inapodhoofika mzungumzaji hutumia nguvu kidogo kuitamka (Wa Mberia, 1993; Mgullu, 1999; Mwembu, 2012). Mfanyiko huu unajitokeza katika Kĩĩtharaka kupitia baadhi ya maneno katika ngeli ya 12/13.

| 3 (a) | **Umoja** | **Wingi** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| | /ka+uŋga/ [kauŋga] | /tu+ uŋga/ [tu:ŋga] | ‘kitoto/vitoto ( vya nyuni)’ |
| | /ka+rigi/ [kariɤi] | /to+riɤi/ [kariɤi] | ‘kamba ndogo(umoja/wingi)’ |
| | /ka+rema/ [karema] | /to+rema/ [torema] | ‘kilima/vilima’ |
| | /ka+urɔ/ [ka+urɔ] | /tu+urɔ/ [tu:rɔ] | ‘kijito/vijito’ |
| | /ka+remɛ/ [karemɛ] | /toremɛ/ [toremɛ] | ‘kilimi/vilimi’ |

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.860

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 (b) | /ɤa+cui / [ ɤacui] | /to+cui / [tocui] | 'kifaranga/vifaranga' |
| | /ɤa+cɛmbɛ/ [ɤacɛmbɛ] | /to+cɛmbɛ/ [tocɛmbɛ] | 'kijembe/vijembe' |
| | /ɤa+te/[ɤate] | /to+te/ | 'kijikiti/vijikiti' |
| | /ɤa+to:ra/[ɤato:ra] | /to+to:ra/[toto:ra] | 'kijiji/vijiji' |
| | /ɤa+ka:re/[ɤaka:re] | /to+ka:re/[ɤaka:re] | 'kijigari/vijigari' |

Katika ngeli ya 12/13 kiambishi awali ni {ka} na {tu/to} mtawalia kama inavyodhihirika katika (3a). Hata hivyo, katika (3b) kiambishi awali cha ngeli 12/13 ni {ɤa} na {tu/to} katika uchanjari huo. Katika umbo ndani, kiambishi awali cha ngeli 12 kinatarajiwa kuwa {ka}, lakini kinatokea kama {ɤa} katika umbo nje. Kwa hivyo, sauti /k/ inadhoofika inapobadilika kuwa /ɣ/. Hii ni kwa sababu sauti /ɣ/ ni ghuna na huhitaji nguvu kidogo kutamka ikilinganishwa na sauti /k/ inayohitaji nguvu nyingi kutamka kwa kuwa sighuna. Itabainika kuwa mfanyiko huu unatokea katika maneno ya ngeli 12 ambayo mzizi wa neno huanza kwa sauti sighuna. Hivi ni kusema kwamba katika mfumo wa sauti za Kîîtharaka iwapo neno limeundwa na mzizi unaoanza kwa sauti sighuna kiambishi cha ngeli 12 kitakuwa ni {ka}.

**Usilimisho**

TUKI (1990) usilimisho ni kufanana kwa vitamkwa kwa kiasi au kikamilifu kutokana na kuathiriana. Vitamkwa huathiriana kwa kutokea katika mazingira sawa. Usilimisho ni mfanyiko wa kifonolojia unaorahisisha kutamkwa kwa maneno ili kuleta iktisadi. Usilimisho hufanya sauti ikaribiane kimfanano na sauti iliyo jirani yake. Yaani mzungumzaji hahitaji nguvu nyingi kutamka vitamkwa (Massamba, 2011). Kuna aina mbili kuu za usilimisho: Usilimisho mbele na usilimisho nyuma (Katamba, 1993). Katika usilimisho mbele, kitamkwa kilichotangulia huathiri kile kilicho mbele yacho.

Kîîtharaka kina mfanyiko wa usilimisho. Aina ya usilimisho unaopatikana katika Kîîtharaka unajulikana kama usilimisho pamwe (TUKI,1990; Mberia,1993; Mgullu, 1999). Kiambishi kiwakilishi cha mtenda, nafsi ya kwanza umoja ambacho ni {ni} kinapotangulia mzizi wa kitenzi unaoanzia kwa konsonanti, ubadili sauti wa aina mbili hutokea. Kwanza, irabu katika {ni} hudondoshwa, na pili, kunatokea usilimisho pamwe wa sauti /n/ kwa kutegemea konsonanti inayoitangulia. Hii hapa mifano ya Kîîtharaka.

| | | |
|---|---|---|
| 4. | /ni+buk+ɛ/→[mbukɛ] | 'nifukue' |
| | /ni+cɔky+ɛ/→ [ɲcɔkyɛ] | 'nirudishe kitu mahali' |
| | /ni+jyty+ɛ/→[ɲɟyetyɛ] | 'nihape' |
| | /ni+kam+ɛ/→[ŋkamɛ] | 'nikame' |
| | /ni+ɣwat+ɛ/→[ŋgwatɛ] | 'nishike' |

Katika 5 konsonanti /n/ inabadilisha mahali pake pa kutamkiwa; ambapo ni ufizi; na kuanza kutamkiwa katika mahali sauti inayoiathiri inatamkiwa. Yaani, kunatokea mfanyiko aina ya usilimisho pamwe. Hali hii hutokea baada ya kutokea mfanyiko wa udondoshaji irabu ambapo irabu /i/ hudondoshwa.

**Uyeyushaji**

Ubadili sauti wa aina hii unahusisha irabu mbili tofauti kubadilika na kuwa kiyeyusho. Katika Kîîtharaka, Mfanyiko huu husababisha kutokea kwa kiyeyusho /w/.

| | | |
|---|---|---|
| 5. /mo+aŋki/→[mwaŋki] | 'moto' | Ng.3 |
| /mo+ɛŋgɛrɛ/→[mwɛŋgɛrɛ] | 'mwanya' | Ng.3 |
| /mo+amba/→[mwamba] | 'mwizi' | Ng.1 |
| /mo+aki/→[mwaki] | 'mjenzi' | Ng.1 |

Nomino katika ngeli ya 1na 3 hutarajiwa kuwa na kiambishi ngeli kilicho na umbo {mû}. Hata hivyo, kutokana na mvutano wa irabu mbili zinazofuatana wakati kiambishi {mû} kinapotangulia irabu inayoanza katika mzizi wa nomino ya ngeli mbili husika, kunatokea uyeyushaji. Katika hali hii kiyeyusho /w/ hupatikana. Hali kama hii pia hupatikana katika baadhi ya nomino katika ngeli ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.860

13. Kwa mfano /to+are/→ [tware] 'wasichana wachanga'.

**Uchopekaji wa Sauti**

Huu ni mchakato wa kuongezea irabu au konsonanti katika neno ili kufuata muundo wa fonolojia wa lugha fulani. Muundo wa silabi wa Kĩĩtharaka kama ilivyo lugha nyingi za Kibantu ni #(V)KVKV…V#. Mara nyingi silabi wazi ndiyo hujitokeza (Gichuru, 2020). Maneno mkopo yanapoasilishwa katika Kĩĩtharaka hulazimu yafuate muundo wa silabi wa KV/V. Kwa mfano katika uasilishaji wa neno mkopo *clinic* kutoka Kiingereza (KKV+KVK) inalazimu mzungumzaji kuchopeka irabu katikati ya konsonanti mbili katika silabi ya kwanza na pia katika silabi ya pili ili neno hilo liwe *kîrînîki*. Hivyo basi, neno husika likachukua muundo wa KV+KV+KV+KV. Ni muhimu kutaja kwamba mengi ya maneno yaliyokopwa kutoka Kiingereza yamekumbwa na mchakato wa uchopekaji wa irabu. Hii ni kwa sababu lugha ya Kiingereza ina maneno mengi yenye silabi funge. Kwa hivyo inakuwa shuruti yachopekwe irabu ili yachukue muundo wa silabi wazi ambao ndiyo unaopendelewa na Kĩĩtharaka (Mwembu, 2012).Katika leksia asilia za Kĩĩtharaka kuna mifano inayodhihirisha uchopekaji wa sauti kwa kutegemea lahaja inayotumiwa na mzungumzaji. Kwa mfano:

| 6. | **Neno** | **Maana** | **Lahaja** |
|---|---|---|---|
| *(a)* | *mû+ **ɵ**û+ nga* [mo:ŋga] | 'mgunga' | Kĩĩgoki |
| | *mû +**g**û+nga* [moɤoŋga] | 'mgunga' | Gĩgatue |
| *(b)* | *nwe+ɵe*[nwɛ:] | 'ni yeye' | Kĩgatue |
| | *nwe+**g**e*[nwɛgɛ] | 'ni yeye' | Gĩntugĩ |
| *(c)* | *me+ɵe+mbe*[mɛ:mbɛ] | 'maembe' | Kĩgatue |
| | *ma+**g**e+mbe*[maɤɛmbɛ] | 'maembe' | Gĩntugĩ |

Sauti /ɣ/ imechopekwa katika leksia [mo:ŋga] , [nwɛ:]na [mɛ:mbɛ] katika (6) ili kuvunja mfuatano wa irabu mbili. Ibainike wazi kwamba uchopekaji wa konsonanti unajidhihirisha katika maneno ya kimsingi na pia maneno mkopo katika lahaja zote nne za Kĩĩtharaka. Yamkini kuna baadhi ya maneno katika Kĩĩtharaka ambayo hayajapitia mageuko kamili ili yachukue muundo wa KV.

**Hapololojia**

Silabi nzima ya neno inapodondoshwa katika neno, mfanyiko unaotokea ni hapololojia. Silabi hudondoshwa kwa kuwa imetokea katika mazingira ya ujirani ambamo mna silabi nyingine inayokaribiana nayo sana kimatamshi. (Crowley na Bowern, 2010; Gichuru, 2020).Mchakato wa hapololojia upo katika Kĩĩtharaka.

| 7. | **Umbo ndani** | **Umbo nje** | |
|---|---|---|---|
| (a) | /ni+nint+er+a/ → | [nintera] | 'niletee' |
| | Silabi 4 | silsbi 3 | |
| (b) | /ni+rɛt+ɛr+a/ → | [ndɛtɛra] | 'niletee' |
| | Silabi 4 | silabi 3 | |

Katika 7 (a) umbo ndani la neno [nintera] ni [ninintera]. Hii ni kwa sababu mzizi wa neno hili ni {-nint-} na kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja ni {ni}. Kwa hivyo, silabi $ni$ ya kiwakilishi cha nafsi ya kwanza kikikaribiana na silabi $ni$ ya mzizi wa neno hili ambao ni {-nint-}, kunatokea udondoshaji wa silabi moja kati ya hizi ambazo zinafanana kimatamshi na pia zimo katika mazingira yanayokaribiana. Katika hali hii umbo nje la neno husika katika mnyambuliko wa kutendea ni [nintera]. Katika 7 (b) kunatokea hapololojia baada ya kutokea mfanyiko wa udondoshaji wa irabu /i/ na hatimaye kuimarika kwa fonimu /r/ wakati inapobadilika na kuwa sauti /d/ kama ifuatavyo /ni+rɛt+ɛr+a/→ [ndɛtɛra]. Katika mifano yote miwili 7 (a) na (b) kila neno linapoteza silabi moja moja linapokuwa katika umbo nje.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.860

**Kanuni ya Ganda katika Kîîtharaka**

Katika Kîîtharaka, kuna ubadili wa kifonolojia ambao matokeo yake yana misingi katika Kanuni ya Ganda. Kanuni hii iligunduliwa na mwanaisimu Mjerumani kwa jina Carl Meinhof. Kwa mara ya kwanza ilidhihirika katika lugha ya Luganda huko Uganda, ndiposa ikaitwa Kanuni ya Ganda.Hata hivyo, ubadili wa sauti unaojitokeza katika kanuni hii hutokea katika lugha kadha za Kibantu zinazozungumzwa katika Afrika Mashariki. Kanuni ya Ganda inasema kuwa: Ikiwa shina la neno linaanza kwa konsonanti ambayo inatangulia mfuatano wa irabu na konsonanti; na iwe kwamba konsonanti hiyo imetanguliwa na king'ong'o; basi konsonanti inayoanza katika shina hudondoshwa (Mberia, 1993; Peng, 2007). Hii hapa mifano inayothibitisha kwamba Kanuni ya Ganda inajitokeza na kutumika katika Kîîtharaka.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8.(a) | [ŋɔmbɛ] | | 'ng'ombe' |
| | [ŋɔndu] | | 'kondoo' |
| | [ŋina] | | 'mamake' |
| 8. (b) | /n+ɣɔmbɛ/ | → | [ŋgɔmbɛ] |
| | /n+ɣɔndu/ | → | [ŋgɔndu] |
| | /n+ɣina/ | → | [ŋgina] |
| (c) | /ŋgɔmbɛ/ | → | [ŋɔmbɛ] |
| | /ŋgɔndu/ | → | [ŋɔndu] |
| | /ŋgina/ | → | [ŋina] |

*Asili*: Mberia (1993:95)

Katika (8a) ni umbo nje la leksia *'ng'ombe', 'ng'ondu'* na *'ng'ina'*. Hili ndilo umbo linalotamkwa na kuandikwa. Hata hivyo, kabla ya kupata umbo hili, leksia husika huwa zimepitia mifanyiko inayoathiri umbo ndani mpaka kukapatikana umbo nje. Katika (8b) kunatokea ubadili wa usilimisho pamwe wakati king'ong'o /n/ kinapoathiriwa kimatamshi na kuanza kutamkiwa kwenye sehemu inayotumika kutamkia sauti /ɣ/ (g). Hata hivyo, baada ya mfanyiko wa usilimisho pamwe, Kanuni ya Ganda inajitokeza katika (8c). Konsonanti /ɣ/ inaanza katika shina na kisha inatanguliwa na king'ong'o /ŋ/ na wakati huo uo inafuatiwa na irabu zikiwa katika mfuatano na konsonanti. Mpangilio wa vitamkwa wa aina hii unasababisha kudondoshwa kwa sauti /ɣ/. Ubadili ya aina hii unaweza kuelezwa kwa misingi ya Kanuni ya Ganda.

**Kanuni ya Dahl katika Kîîtharaka**

Kanuni ya Dahl hutumiwa kueleza mfanyiko wa kimsigano unaokumba sauti sighuna katika idadi fulani ya lugha za Kibantu zinazopatikana katika Afrika Mashariki. Kanuni hii ilipewa jina kutokana na Edmund Dahl aliyeigundua katika lugha ya Kinyamwezi. Kanuni ya Dahl inapatikana katika lugha za kundi la Thagicu, ingawa si kila lugha ya kikundi hiki huwa na mfanyiko huu. Zaidi ya hayo, hata katika lugha ambazo mfanyiko huu hutokea, kuna mipaka yake (Bennett, 1977). Kanuni hii inadai kuwa kipasuo cha kiambishi awali ambacho katika umbo ndani huwa sighuna hubadilika kuwa ghuna ikiwa shina au kiambishi kinachofuata kimeanza kwa sauti sighuna. Katika hali, kunatokea msigano wa sauti katika kiambishi awali kwa kutokea sauti ghuna katika shina la neno. Sauti /k/ ndiyo mara nyingi hukumbwa na mfanyiko huu. Hata hivyo, katika baadhi ya lugha, sauti nyingine kama vile /t/, /p/, /c/, /nt/ŋk/, /ɲc/na /mp/ huathiriwa na mfanyiko huu (Mberia, 1993; Uffmann, 2013). Katika Kîîtharaka, mifano ifuatayo inathibitisha mfanyiko unaofuata Kanuni ya Dahl.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 9. (a) | /k/ | /ko+kɛð+a/ | → | [ɣokɛða] | 'kuvuna' |
| | | /ko +ko:ra/ | → | [ɣoko:ra] | 'kung'oa' |
| (b) | /c/ | /ko+cimb+a/ | → | [ɣocimba] | 'kuchimba' |
| | | /ka+ciati/ | → | [ɣaciati] | 'ufagio mdogo' |
| (c) | /t/ | /ko+twir+a/ | → | [ɣotwira] | 'kulisha mifugo katika boma' |
| | | /ko+tɛð+i+a/ | → | [ɣotɛðia] | 'kusaidia' |
| (a) | /nt/ | /ke+nto/ | → | [ɣento] | 'kitu' Ng.7 |

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.860

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | /ka+nto/ | → | [ɣanto] | 'kitu' Ng.12 |
| (b) /ŋk/ | /ka+ŋkena/ | → | [ɣaŋkena] | 'jina la ukoo' |
| | /ko+aŋkan+w+a/→ | | [ɣwaŋkanwa] | 'kuhisi maumivu' |
| (c) /mp/ | /ko+ump+a/ | → | [ɣumpa] | 'kushambulia' |
| | /ka+umpu/ | → | [ɣaumpu] | 'kitita' |
| (d) /ɲc/ | /ko+incj+a/ | → | [ɣwincja] | 'kufumba macho' |
| | /ka+inci/ | → | [ɣainci] 'uzio mdogo wa miba' | |
| (e) /p/ | /ka+pakɔ/ | → | [ɣapakɔ] | 'kishikio' |
| | /ka+pampɔ/ | → | [ɣapampɔ] | 'sisimizi' |

Kwa kuzingatia mifano ya leksia katika (9), inabainika kwamba Kanuni ya Dahl inatenda kazi kwa njia inayoathiri sauti /k/. Kwa ufupi, ubadili unaojitokeza katika sauti za Kîîtharaka kwa misingi ya kanuni hii ni kuwa, kitamkwa /k/ katika kiambishi awali katika umbo ndani hubadilika kuwa /ɣ/ ikiwa konsonanti ya kwanza ya shina la neno ni sauti sighuna.

## UBADILI WA KIMOFOLOJIA KATIKA KÎÎTHARAKA

Mofolojia ni tawi la isimu ambalo huchunguza maneno na aina zake (TUKI, 1990).Richards na wenzake (1985) wanasema kuwa mofolojia ni taaluma ya isimu inayochunguza mofimu na alomofu zake na jinsi ambavyo hukaa pamoja kuunda maneno mbalimbali katika lugha zinamotumika. Kutokana na vijelezo hivi ni kwamba, mofolojia ni taaluma katika ngazi za kiisimu yenye jukumu la kuchunguza na kuchambua maumbo ya maneno kwa nia ya kuelewa maana ya kila mofimu. Kwa hivyo, utafiti huu unapojishughulisha na ubadili wa kimofolojia unaangazia vipashio mbalimbali vya lugha kama vile mofu, alomofu na mofimu ambavyo ndivyo vijenzi vikuu vya neno.

### Ubadili Unaoathiri Mofu za Ngeli

Mofu ni kipashio cha chini kabisa chenye maana katika lugha. Mofu haiwezi kuvunjwavunjwa zaidi bila kupoteza maana. Maana za kisarufi na kileksia huwa katika mofu (Platt, 1985). Kwa mujibu wa Mgullu (1999), mofu ni umbo la neno ambalo huwakilisha mofimu. Umbo hili hudhihirika kifonolojia na kiothografia. Mofimu ni vipashio vya kidhahania ambavyo huwakilishwa na mofu zinazodhihirika kifonolojia zikiwa ni sauti za kutamkwa au kiothografia zikiwa ni alama za kuandikwa. Mofimu moja inaweza kuwakilishwa na maumbo tofauti ya mofu moja, yaani alomofu. Alomofu ni umbo mojawapo kati ya maumbo kadhaa tofauti yanayowakilisha mofimu moja (Richards na wenzake, keshatajwa). Alomofu pia inaweza kuwa mofu mojawapo katika seti ya mofu zinazowakilisha mofimu fulani ambayo ina mahali mahususi ya kifonetiki, kileksia au kisintaksia inamotokea (Bauer, 1983; Mgullu, keshatajwa).

Katika Kîîtharaka kuna ubadili unaoathiri mofu za maneno kwa njia moja au nyingine. Mofu {mû} inayowakilisha ngeli 1 hupitia ubadili na kujitokeza kama alomofu tatu ambazo ni: {mû}, {mu} na {mw). Mfano wa maneno kama haya ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10. (a) | {mû+rîmi}→mûrîmi | 'mkulima' | Ng.1 |
| | {mû+rîthi}→mûrîthi | 'mchungaji' | Ng.1 |
| | {mû+rori}→mûrori | 'mrinaji' | Ng.1 |
| (b) | {mu+ntû}→muntû | 'mtu' | Ng.1 |
| | {mu+ngania}→mungania | 'anayechanganya vitu'Ng.1 | |

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.860

| | | | |
|---|---|---|---|
| (c) | {mw+ana}→mwana | 'mtoto' | Ng.1 |
| | {mw+aki}→mwaki | 'mjenzi' | Ng.1 |
| | {mw+amba}→mwamba | 'mwizi' | Ng.1 |

Ubadili wanayoathiri mofu {mû} na kuzalisha alomofu {mw} katika ngeli 1, vilevile ndiyo husababisha mofu {mû} ya ngeli 3 kuwa na alomofu {mw}.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. (a) | {mû+tî} | →mûtî | 'mti' | Ng. 3 |
| | {mû+konge} | →mûkonge | 'mkonge' | Ng.3 |
| | {mû+ramba} | →mûramba | 'mbuyu' | Ng.3 |
| (b) | {mw+atû} | →mwatû | 'mzinga' | Ng.3 |
| | {mw+anya} | →mwanya | 'mwanya' | Ng.3 |
| | {mw+anki} | →mwanki | 'moto' | Ng.3 |

Alomofu {mw} katika Ng.1&3 hutokana na mfanyiko wa uyeyushaji ambao husababishwa na mvutano wa irabu /o/ na /a/. Irabu /o/ ni ya nyuma juu kati, huku irabu /a/ ni ya chini. Kwa hivyo inakuwa vigumu kutamka sauti hizi kwa mfuatano. Katika hali hii, kiyeyusho /w/ ambacho ni rahisi kutamkika kikifuatana na irabu /a/ huchukua nafasi ya irabu /û/. Hata hivyo, ubadili wa mofu {mû} kuwa alomofu {mw} katika Ng.1&3 yanaweza kutatanisha mtu mgeni anayejifunza Kîîtharaka.

Kwingineko, katika Ng.2, kiambishi kiwakilishi cha ngeli ambacho ni {a} kina alomofu {e} kama ilivyo katika (12).

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. (a) | {a+ntû] | → antû | 'watu' |
| | {a+rimo} | → arimo | 'walimu' |
| | {a+ciar+i} | → aciari | 'wazazi' |
| (b) | {a+ekuru} | → ekuru | 'akina mama' |
| | {a+endia} | → endia | 'wauzaji' |
| | {a+endi} | → endi | 'wenye nia' |

Kimsingi, maneno katika ngeli ya 2 yanatarajiwa kuanza kwa mofu {a} kama ilivyo katika (12a). Hata hivyo, katika (12) (b) mofu hii inajitokeza kama {e}. Ubadili huu unatokana na udondoshaji wa mofu {a} na hivyo kubadilisha dhima ya sauti /ɛ/ ili kuwa mofu ya kuwakilisha ngeli 2. Vilevile, mofu inayowakilisha ngeli ya 8 ambayo ni {î} ina alomofu {î} na {bi} kama ilivyo katika maneno *îratu* 'viatu', *itheti* 'mikoba', *biama* 'miujiza', *biara* 'vidole'. Alomofu {bi} hutokea katika mazingira ambapo shina la nomino huanza kwa irabu. Sababu ya matokeo haya ni ya kifonolojia. Muundo wa silabi unaopendelewa na Kîîtharaka ni wa KV, kwa hivyo, iwapo silabi mbili zinazoundwa na irabu pekee zinafuatana inabidi konsonanti ichopekwe mwanzani mwa neno ili kuafiki muundo wa KV. Kwa mfano.

{-ama}→{î+ama}→{iama}→{b+i+ama}→{biama}

**Ubadili Unaoathiri Mofu za Ukanusho**

Mofu ya ukanusho katika Kîîtharaka huwa ni {ti}. Mofu hii hujitokeza katika nafsi zote tatu hali ya umoja na wingi. Hata hivyo, kuna ukiushi hapa na pale. Ukiushi huu husababishwa na ubadili wa mumo kwa mumo unaotokea katika neno mpaka kukapatikana alomofu {ti}, {ta} {nti} na {nta} ambazo ni maumbo tofauti ya mofu {ti}. Kwa mfano.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.860

| | | Uyakinisho | | Ukanusho | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 13. (a) | (i) | akarîma | → | a**ti**rîma | 'hatalima' |
| | (ii) | akathi | → | a**ti**thi | 'hataenda' |
| | (iii) | agûtema | → | a**ti**ratema | 'hajakata' |
| | (iv) | nakûrîma | → | a**ti**kûrîma | 'halimi' |
| | (v) | nararîmire | → | a**ti**rarîma | 'hakulima' (wakati uliopita jana) |
| (b) | (i) | ndarîmire | → | **nta**rîma | 'sikulima' (wakati uliopita juzi na zamani) |
| | (ii) | ndararîmire | → | **nti**rarîma | 'sikulima' (wakati uliopita jana) |
| | (iii) | ndîmire | → | **nti**rarîma | 'sikulima' (wakati uliopita siku hiyo) |
| (c) | (i) | n'arîmire | → | a**ta**rîma | 'hakulima' (wakati uliopita juzi na zamani) |
| | (ii) | ibaarîmire | → | ba**ta**rîma | 'hawakulima' (wakati uliopita juzi na zamani) |
| | (iii) | ibwarîmire | → | bu**ta**rîma | 'hamkulima'(wakati uliopita juzi na zamani) |

Katika (13a) mofimu ya ukanushaji inawakilishwa na alomofu {ti} huku alomofu {nti}, {nta} na {ta} zikiwakilisha mofimu iyo hiyo katika (13b) na (c) mtawalia. Kimsingi, mofu inayotarajiwa kuwakilisha dhana ya ukanushaji katika Kîîtharaka ni {ti}. Hata hivyo katika (14b) kwa mfano, kunatokea ubadili ambao unasababisha kupatikana kwa alomofu {nti} na {nta}. Katika hali hii, leksia katika (13b) (i) (ii) (iii) zimepitia mchakato kwa njia hii:

{ni+ti+nda+rîm+ir+e}→ {ni+ti+a+rîm+ir+e}→{nti+a+rîm+ir+e}→{nta+rîm+a}→ {ntarîma}

{ni+ti+nda+ra+rîm+ir+e}→{ni+ti+a+ra+rîm+ir+e}→{nti+ra+rîm+ir+e}→{nti+ra+rîm+a}→{ntirarîma}

{ni+ti+nda+ra+rîm+ir+e}→{ni+ti+a+ra+rîm+ir+e}→{nti+ra+rîm+ir+e}→{nti+ra+rîm+a}→{ntirarîma}

Katika ubadili haya, mofu {ni} ambayo inawakilisha nafsi ya kwanza umoja inashirikiana na mofu {ti} ya kukanusha ili kuunda alomofu {nti} au {nta}. Hii ni baada ya kudondoka kwa mofu nyingine ambazo hazipaswi kuwa katika leksia husika ikiwa katika hali ya kukanusha.

## Ubadili wa Kisarufi katika Mofu za Uambishaji

Mofu za uambishaji katika lugha ambishi-bainishi huwa hazichanganyikani na mizizi ya maneno, na ni rahisi kubainika katika neno. Kila mofu inayoambishwa huwa na maana ya kisarufi moja au zaidi (Mgullu,keshatajwa). Katika Kîîtharaka, kuna mofu zinazobeba maana tofauti za kisarufi kwa kutegemea muktadha wa mazungumzo. Kwa mfano,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14. (a) | (i) | andîk+**an+**a | →{andîkana} | 'andikana'/patiana ujira' |
| | (ii) | kw+andîk+**an**+a | →{kwandîkana} | 'kuajiri'/kuweka orodha ya majina ya watu' |
| (b) | (i) | mw+andîk+**an+i** | →{mwandîkani} | 'mwajiri' |
| | (ii) | gw+andîk+**an+i** | →{gwandîkani} | 'mchakato wa kutoa ajira' |

Mofu {an} katika (14 b) (i) na (ii) inawakilisha maana mbili mbili za kisarufi. Katika (14 a) (i) inawakilisha kauli ya kutendana, na vile vile kitendo cha kutoa ajira. Katika (14 a) (ii) mofu ile ile na katika mazingira yale yale, lakini inawakilisha maana ya kisarufi tofauti na jinsi ilivyo katika (14 a) (i). Tofauti hizi zinajidhihirisha kwa njia mbili. Kwanza, mofu {an} inaposhirikiana na mofu {kw} inabadili maana ya kisarufi inayoashiria kauli ya kutendana na kuleta dhana ya kutoa ajira kwa mtu fulani. Pili, mofu hii inawakilisha dhana ya kurekodi majina ya watu kwa kusudi maalum. Katika (14 b) (i) na (ii) mofu {an} inatumika kuleta ubadili maana kwa kuwa (iii) inaashiria mtu anayewapa watu ujira, yaani mwajiri, huku katika (ii) ikionyesha mchakato wa kuajiri watu kazi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.5.1.860

Katika hali hii, mofu {an} inatumika katika vitenzi kuleta maana tofauti na ile inayojitokeza katika nomino.

## HITIMISHO

Makala haya yanahitimisha kwamba mabadiliko ya sauti na mofu katika leksia za lugha huathiri maana ya neno kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja. Uelewa wa kisemantiki wa leksia huanzia katika akili ya mzungumzaji anapojenga picha kuhusu maana ya sauti na mofu zinazojenga neno husika. Data iliyowasilishwa katika makala haya inadhihirisha kuwa kuimarika kwa fonimu, kudhoofika kwa fonimu, uchopekaji wa sauti, hapololojia na mabadiliko katika mofu zinazowakilisha maana za kisarufi mbalimbali huwa na mchango katika matokeo yanayotokana na ubadili maana katika leksia za Kîîtharaka.

## MAREJELEO


Bauer, L. (1983). *English Word Formation.* Cambridge: Cambridge University Press.

Bennett, R.P. (1977). Dahl's Law andtheThagicu. In*African LanguageStudies,* Vol. VII, pp. 127-159.

Bennett, R.P. (1985). DhaagicwLifeStages: A StudyinParadigmaticReconstruction. In *HistoryinAfrica*, Vol 12 pp. 11-28.

Blutner, R. (1990). Lexical Pragmatics in *Journal of Semantics*; Vol. 15 (2) Pp. 115-162 katika tovuti https:/www.blutner.de/iex.pragpdf, accessedon 23/9/2020.

Crowley, T.,&Bowern, C. (2010). *An Introduction to Historical Linguistics.* London: Oxford.

Gichuru, T. M. (2020). Mabadiliko ya Maana za Leksia za Kiswahili: Mtazamo Linganishi wa Kale na Kisasa. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Guthrie, M. (1970). *The Classification of Bantu Languages,* London: International African Institute.

Katamba, F. (1993). *An Introduction to Phonology*. London: Longman.

Massamba, D.P. (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mberia, K. (1993). Kîîtharaka Segmental Morphophonology with special reference to the Noun and Verb. (Unpublished) PhD. Thesis.University of Nairobi.

McMahon, A.M.S. (1994). *Understanding Language Change*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mgullu, R. (1999). Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mukuthuria, M. (2004). Kuathiriana kwa Kiswahili na Lahaja ya Kitigania: Uchanganuzi wa Taathira katika Muktadha wa Shule za Msingi na Upili katika Tigania-Kenya. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton.

Mwembu, K.N. (2012). *Uasilishaji wa Maneno ya Kigeni katika Lahaja ya Kîîtharaka, Kenya*. Tasnifu ya uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuka.

Peng, L. (2007). Geminationand Anti-Gemination: Meinhof's Law inLuGandaand Kikuyu.

Richards, J.C. na Wenzake (1985). *Dictionary of Applied Linguistics*. Harlow: Longman.

TUKI, (1990).*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributers Ltd.

Uffmann, C. (2013). Set the Controls for the Heart of the Alteration: Dahl's Law in Kîîtharaka. *Nordlyd* Vol 40.1 pp 323-337.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.